**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**KIDATO CHA 3**
**JULAI/AGOSTI 2024**

# ***MWONGOZO WA KUSAHIHISHA***

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1**

a)
- Ni majigambo / vivugo
- Matumizi ya mimi ni….. **(1x2)**

b) Ni wafugaji – nilipokuwa nalisha mifugo
Ni wezi wa mifugo – mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Wanajihusisha na vita **(2x1)**

c) - Istiara (sitiari) Ni mimi Jabali
- Tashbihi – Kasi kama umeme
  Ulipaa kama umeme
  Kama mmweso wa radi
- Mdokezo – mifugo ikanifuata…
- Swali la balagha – mmekuwa kama majivu baada ya jua moto kuzimika?
- Chuku – upanga kupasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
- Msemo – kufumba na kufumbua
- Urudiaji (takriri) nikachukua mkuki wangu
  Nikachukua upanga wangu

Matumizi ya mishororo mishata m.f wazee waliposhindwa
Nilipokuwa nalisha mifugo…
- Uhuishi – mkuki kupaa
- Usambamba – nikachukua mkuki wangu, nikachukua upanga wangu

d) - Anayejigamba hutunga kufuatia tukio mahususi katika maisha yake – anakumbuka alivyokomboa mifugo ya Mtemi kutoka kwa wezi
- Huwa na matumizi ya chuku
- Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na wanaume
- Hutolewa kwa nafasi ya kwanza m.f Nikachukua mkuki wangu
- Anayejisifu huweza kutaja usuli wake wa kinasaba m.f Ochilamgwara mwana mbee wa Ojilong
- Maudhui makuu ni ushujaa
- Hutungwa kwa usanii mkubwa – sitiaru urudiaji tashbihi n.k

e) - Avae maleba – mkuki, upanga ngozo
- Atumie kiimbo na toni kupanda na kushuka kwa sauti yake
- Atumie miondoko ya mwili
- Atumie ishara za uso
- Ashirikishe hadhira kwa kuuliza maswali ya balagha

**Kadiria hoja Zaidi (za kwanza 4x1=4)**

f) - Kufanya utafiti Zaidi
- Kuhifadhi kwenye kanda tepu rekodi video n.k
- Kufunza shuleni
- Kupanga mashindano kati ya jamii mbalimbali
- Kuhifadhi katika maandishi
- Kuhimiza watu kutunga tungo kama hizi
- Sherehe mbalimbali

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**B.USHAIRI**

**2.**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 1)

***- Binadamu hatosheki/ binadamu ana tamaa/tamaa ni hatari***

b) Fafanua mambo matatu ambayo hafsineni analalamikia (alama 3)

***- Mtu aliye na tamaa huwa hatari kama nyoka***

***- Unafiki wa mtu asiyeaminika***

***- Masengenyo***

***- Balaa ya kumkirimu mchawi ni kutupiwa kinyesi***

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo (alama 3)

(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo

***- Ukawafi/tumbuizo – Kila mshororo una vipande vitatu – ukwapi, utao, mwandamizi ambavyo vinatoshana kwa urefu – kila kimoja kina mizani nane***

(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti

- ***Ukaraguni –vina vya kila kipande vinatofautiana katika shairi nzima***

(iii) Idadi ya mshororo katika kila ubeti

***- Tarbia – Kila ubeti una mishororo minne***

d) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari (alama 4)

***- Ni taabu kuishi na mtu aliye taraghani kwani kazi yake ni kujidai***

***- Atakusema faraghani asivyosema ukiwa naye kuwapendeza maadui zako***

***- Ni mtu akuchimbaye. Hana faida nyumbani bora usimtegemee***

***- Mtu aliye na tamaa ya kutaka kisicho chake ni hatari kama nyoka***

e) Bainisha tamadhali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)

***- Tashbihi/tashbiha – ni hatari kama nyoka***

***- Tashihisi/uhaishaji/uhuishi – bahati inahadaa bahati kupewa uwezo wa kudanganya***

***- Litifati – Subutu' kumwacha mtu ajisemee***

***- Jazanda /sitiari Kinyesi nimetupiwa***

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama 2)

***- Inkisari – ukweliye badala ya ukweli wake, kiso badala ya kisicho n.k***

***- Miundo ngeu ya kisintaksia/ kuboronga sarufi/kufinyanga sarufi – ninacho changu kilio badala ya ninacho kilio changu***. (za kwanza 2x1=2 ataje, atolee mfano na asahihishe au atuzwe 0)

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)

***- Urudiaji wa neno – kweli***

***- Urudiaji wa sauti – a-balaa, hadaa, jaa, tamaa***

***- Urudiaji wa mstari- mtu kuwa na tamaa. Akitaka kiso chake. Ni hatari kama nyoka***

***- Urudiaji wa silabi – Ki, ki, ki*** (za kwanza 2x1=2 atolee mfano au atuzwe 0)

h) Fafanua muundo wa ubeti wa tano (alama 3)

***- Mistari/mishororo minne katika ubeti***

***- Vipande vitatu katika kila mshororo***

***- Vina vyake ni: a, wi, yo***

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

*- Mizani 8,8,8 = 24 katika kila mshororo*
*- Mshororo wa mwisho unarudiwarudiwa/kibwagizo (lazima atolee mfano mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake,ni hatari kama nyoka.*

**3.**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha (al. 2)
**Shairi huru – halijazingatia kanuni zote za utunzi wa mashairi wa kuzingatia arudhi.**

b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili (al. 2)
- **Anayeimba ni mjomba**
- **Anayeimbiwa ni mpwawe**

c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume(al. 2)

- **Anaambiwa uoga ukimtikisa huenda ni wa akina mamaye**
- **Alichinjiwa fahali ili awe mwanaume**

d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili al. 4)
- **Chuku – wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo**
- **Takriri – kikali**
- **Isitiari – upweke ni uvundo**
- **Tashhisi – uoga ukifikia**

e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
- **Wakulima – Atapewa shamba la mahindi**
- **Wafugaji – Atapewa mbuzi**

f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi (al. 4)
- **Tabdila- aamushwe – aamshwe**
- **Inkisari – Mme – mwanaume**
- **Kuboronga sarufi – Fahali tulichinja-tulichinja fahali**

g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (al. 4)
- Mbari – **ukoo**
- Msununu – **anayenuna**
- Ngariba – **mtahirishaji**
- Uvundo – **harufu mbaya**

## <u>C.TAMTHILIA-BEMBEA YA MAISHA</u>

4.. “Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilibyoalika sasa”
a) Weka ndodoo hili katika muktadha (alama 4)
*- Maneno ya Dina*
*- Kwa Sara*
*- Wakiwa nyumbani kwa Sara jikoni*
*- Sara alikuwa amemtumia wito Dina aende amsaidie kupika* 4x1=4

b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo (alama 6)
*- Mwenye huruma – anamhurumia Sara jinsi anavyouguza ugonjwa wake*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

*- Mwenye ujirani mwema- anakuwa tayari kumsaidia Sara kama jirani wake*
*- Mwenye roho safi – hamwonei wivu Sara kwa kufanikiwa kwa watoto wake*
*- Mwenye mapenzi ya dhati- hataki wito wa Sara*
*- Ana kumbukumbu nzuri – anakumbuka masaibu ya Sara katika ndoa yake*
*- Ana mlahaka mzuri na mtoto wake Kiwa – anakuja kumjulia hali.* *Zozote 6x1=6*

c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha (alama 10)

*- Sara na Yona wanajaliwa watoto watatu wa kike baada ya muda*
*- Yona anabaki kwa ndoa licha ya shinikizo kutoka kwa wanajamii aoe mke mwingine ili ampe mtoto mvulana*
*- Sara ana jirani kama Dina ambaye anamsaidia kila anapolemewa*
*- Sara anamsaidia Yona kuwasomesha watoto wao alipopoteza kazi ya ualimu*
*- Watoto wao wanahitimu masomo yao hadi chuo kikuu*
*- Neema anaolewa na bwana anayempenda na kumjali –Bunju*
*- Ndoa ya Bunju na Neema inawapa Sara na Yona wajukuu- Lime na Mina*
*- Sara anakuja kuchukuliwa kwa gari na Neema kumpeleka mjini kwasababu ya matibabu*
*- Mjini Sara anapelekwa Hospitali nzuri ya wataalamu wanaoshughulikia ugonjwa wake vilivyo*
*- Neema na Bunju wamewajengea Sara na Yona nyumba*
*- Neema anampa babake Yona pesa za dawa na zamasurufu*
*- Kijijini jina la Neema limeenea kwa sifa ya kuwa mja wa kwanza kuendesha gari kijijini.*
*- Neema anawanunulia wazazi wake kochi jipya*
*- Neema anawanunulia wazazi wake jiko la gesi*
*- Yona anaanza kumjali mkewe Sara kwa kumpikia kiamsha kinywa.*

**5.**. (a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)

*- Nidaa – mke wangu!*
*- Takriri – mwaka baada ya mwaka*
*- Tashihisi – ugonjwa umemla bila huruma*
*- Mbinu rejeshi – jana ningeishi tofauti*
*- Utohozi – silesi - slices*
*- Tashbihi – mfano wa mafuriko msimu wa masika*
*- Nahau – kata shauri*
*- Uzungumzi nafsia – kifungu chote*
*- Ritifaa – anapoisemea pombe*
*- Taswira – umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu/anapunga mkono* *10x1 = 10*

b) Bainisha toni ya dondoo hili (alama 2)

*- Toni ya majuto- Yona anajutia*
*- Toni ya huzuni- Kumtesa mkeweMaskini mke wangu!* *2x1 =2*

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima (ala 8)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Umuhimu wa Yona**

- ***Ametumika kukuza maudhui ya udhalimu kwa kumpiga Sara hadi anapoteza fahamu***
- ***Kupitia kwake tunajua athari za udaku; kusemwa na majirani kwa kutokuwa na mrithi kunampaunyanyapaana kumfanya kugeukia ulevi (uk.9)***
- ***Kielelezo cha wanaume wasiothamini wanawake***
- ***Anakuza ubabedume; hakuthamini Neeme, Asna na Salome kwa kuwa wasichana***
- ***Ametumika kuendeleza bidii anapokuwa mwalimu. Alikuwa anabeba vitabu kwendakusahihisha nyumbani wakati wa wikendi (uk.62)***
- ***Anakuza baadhi ya sifa za Sara (mvumilivu)***
- ***Ametumiwa kujenga mtiririko wa vitushi/ploti ya tamthilia kwa kumpiga Sara, kulewa.***
- ***Anajenga mtindo wa tamthilia kupitia mbinu ya dhihaka, ritifaa, methali. (zozote 4x2=8)***

## D.HADITHI FUPI

**6.**

**Harubu ya maisha** ***Paul Nganga Mutua***

**"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"**

**(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)**

(i) Maneno haya ni ya kikwai

(ii) Anajibu ujumbe wa simu ya Mama Mercy mke wake

(iii) Alikuwa ofisini

(iv) Ilikuwa usiku wa saa nne na bado alikuwa kazini, hofu ya Mama Mercy ni kuwa Mercy angelala bila babake kufika

**(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (al. 6)**

(i) Mwenye mapenzi kwa familia yake – Mama Mercy alipomwambia kuwa Mercy angelala kabla hajafika, aligushwa na kutoka kasi kazini. Pia mamake alipotamka atume pesa nyumbani alisema angetuma.

(ii) Mlezi bora – Anaenda kwa Vaite na kukopa chakula. Anamlisha Mercy. Baada ya kumlisha Mercy, alishindwa kula chakula ilhali Mama Mercy hakula chochote. Hali yake inamfanya kuhisi kulia.

(iii) Mwenye mawazo – Amejawa na mawazo hadi anasahau kumpigia mamake simu. Mama anamjulisha juu ya deni ya yule fundi wa nyumba. Atalazimika kuuza mbuzi, kuku n ahata pesa na deni zikose.

(iv) Mwenue utu – Anamuombea Nilakosi advansi ilhal yeye anahitaji pesa, badala ya kujiombea yeye mwenyewe

(v) Mwenye bidii – Kuendea msaada kwa Kanisa. Pastor alimpa unga uliowashibisha na wakala wakalala. Pia kufanya kazi kwa bidii haa mshahara unapocheleweshwa

(vi) Mvumilivu – Kuvumilia kukosa mshahara, kufokewa na Boss na hata Mama Mercy

**(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (al. 10)**

(i) Kuwa kazini hadi saa nane kasorobo za usiku – Kikuni anapigiwa simu na Mama Mercy kuwa Mercy anamsubiri

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(ii) Usafiri – Usiku hapakuwa na msongamano wa magari barabarani, lakini mchana watu waliotembea kwa miguu, pikipiki na magari yalisongamana
(iii) Kukosa pesa za matumizi. Kikwa analazimika kuenda kukopa chakula kwa Vaite. Yeye na mkewe walilala bila kula. Kulala njaa kwake na mama Mercy pia kulitokana na chakula kilichosalia kuwa kidogo na kunuka mafuta taa.
(iv) Kazi nyingi ya dharura kazini ya kuandaa vitabu kwa ajili ya kuviwasilisha kwenye wizara. Kutumwa na Bosi kumfanyia kazi za kibinafsi kama kumpeleka mtoto wa Bosi hospitalini.
(v) Ukosefu wa mshahara – kukosa kulipwa mshahara kwa miezi miwili
(vi) Uoga – Kuogopa hata kuomba pesa kidogo za matumizi. Hadi Bosi awe kwa 'mood'
(vii) Kutegemewa na jamii – Mama anamjulisha juu ya deni ya yule fundi wa nyumba. Atalazimika kuuza mbuzi, kuku na hata pesa za deni zikoshe kutosha.
(viii) Hali mbaya ya kiuchumu – Bei ya mauzo kushuka na hali ya maisha kupanda.
(ix) Kutembea kuenda na kurudi kutoka kazini kwa sababu ya kukosa pesa za nauli au mafuta ya kuweka kwa gari
(x) Kufanya kazi kwa 'contract' – Nilakosi ambaye mkataba wake unakatika mwezi ujao walitaka kumuachisha kazi sasa.
(xi) Kuomba advansi ya elfu tano – Nilakosi
(xii) Kufungiwa nyumba na Landlord kwa sababu ua kuksa kulipa nyumba. Sababu ni kukosa kulipwa mshahara.
(xiii) Kutumwa kufanya kazi za nyumbani na Bosi – kumpeleka mtoto hospitalini akitumia gari la Kampuni.
(xiv) Kupewa gari na Kampuni lakini kushindwa kuliweka mafuta
(xv) Kufokewa na Bosi – Kikwai alipokosa kuja na gari kazini kwa sababu ya kukosa hela za mafuta ya gari, alimfokea na kumuonya kuwa gari ni lazima liwe pale ofisini.
(xvi) Bosi kukosa kufika ofisini akijua fika kuwa ni mwiso wa mwezi na anafaa kuwalipa wafanya kazi mshahara
(xvii) Bosi katili ambaye anaweza kumlipa Kikwai mshahara wa miezi miwili na kumwachisha kazi ghafla. Kwa hivyo alikuwa na pesa za kumlipa kila mwezi lakini hakufanya hivyo.
(xviii) Kuachishwa kazi kwa ghafla na kulazimika kurudisha kila kitu cha kampuni. Analipwa mshahara wake wa miezi miwili.

**7.Wetu ni wetu,hata akiwa mbaya …ni wetu.Hatuna budi kuchagua yeye .Lisilobudi hubidi.**

**(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)**

- ✓ Ni machoka akikumbuka kauli ya jirani yake zuhura kuwa wanafaa kumchagua mtu wao,awe mzuri au mbaya ,amesoma au la.
- ✓ Machoka ameketi kitako kochini chumbani mwake
- ✓ Baada ya kurejea kutafuta kibarua mchana kutwa bila mafanikio.anajuta kuhusu maamuzi waliyofanya kuchagua viongozi kwa kuegemea nasaba.

**(b) Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili (alama 4)**

- ✓ Methali-lisilobudi hubidi
- ✓ Mbinurejeshi/kisengera nyuma-machoka anakumbuka kauli ya jirani yake zuhura kuwa wanafaa kumchagua mtu wao ,awe mzuri au mbaya ,amesoma au la.anakumbuka hali ya sintohfahamu kati yake na zuhura kutokana na misimamo yao hiyo,hali iliyoyeyushwa na dhiki baada ya uchaguzi.
- ✓ Takriri-''wetu ni wetu,hata akiwa mbaya ni wetu…
- ✓ Kinaya -zuhura anamwambia machoka kuwa wanafaa kumchagua mtu wao,awe mzuri au mbaya.ajabu ni kuwa wao ndio wanateseka chini ya uongozi huo.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**(c) Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.Jadili.**
**(alama 12 )**

- ✓ Ugomvi kati ya zuhura na machoka ni msiba wa kujitakia.wanatofautiana kwa kuwa wana misimamo tofauti katika uchaguzi wa viongozi.Ajabu ni kuwa baada ya uchaguzi ,dhiki inawaleta pamoja kwani viongozi wenyewe hawawajibiki kwa vyovyote vile.
- ✓ Kauli ya zuhura ni ithibati kuwa hali yao ni msiba wa kujitakia.anamwambia machoka kuwa wanafaa kumchagua kiongozi kwa ukoo wao hata kama hafai kwa kuwa ni mtu wao.sasa hivi,zuhura anajutia uamuzi wake huo kutokana na dhiki inayomkumba.
- ✓ Machoka anakumbuka shairi la malenga mteule alilowahi kusoma mahali fulani.shairi hili linahusu msiba wa kujitakia.kibwagizo chake ni ‘’msiba wa kujitakia,kweli hauna kilio’’.linaoana na hali ilivyo katika jimbo la matopeni.linaongelea visanga vilivyojaa nchini watu wakifilisika.mtunzi anamwomba Rabana awafungue macho ili waweze kuona.
- ✓ Machoka anapitia hali ngumu kimaisha .ametoka kutafuta kibarua lakini hajaambulia chochote ,hata cha kutia tumboni.wakazi wengine wa jimbo hili pia wanapitia hali ngumu kama hiyo.hali yao ni msiba wa kujitakia ,kwa kuwa wanafanya uchaguzi bila kuzingatia vigezo vinavyofaa kupata kiongozi anayefaa.
- ✓ Wakazi wa matopeni wanaruhusu jimbo lao kugeuzwa ngome ya watu fulani wanaowania uongozi-wanarauka asubuhi na mapema kustahimili jua la mchana ili kuwapigia kura viongozi ,ambao baadaye wanawapuuza na kutojali matatizo yao.
- ✓ Fumo matata anawakumbusha wakazi wa matopeni kuwa si busara kuwachagua viongozi kwa kuzingatia koo,kwani hali hiyo inaendeleza uongozi mbaya.Hata hivyo ,wanampuuza na kumteua sugu junior kuwa kiongozi.wanazidi kutaabika kutokana na mapuuza yao yao hata baada ya kuonywa.
- ✓ Zuzu matata kukosa uongozi wa matopeni ni msiba wa kujitakia.anapendekezwa na walowezi kutwaa uongozi lakini anasisitiza kuwa lazima sugu senior kwanza aachiliwe kutoka gerezani.anapoachiliwa anakuwa maarufu kumliko na kutwaa uongozi.Anakosa fursa nyingine ya kutwaa uongozi huo wa kubakia kuwa mpinzani wake hadi kifo chake.
- ✓ Wananchi wanakubali kukandamizwa.wanatengewa upande wa kiwanja ulio na jua huku viongozi wakitengewa upande wenye hema na kuongezewa vinywaji na ulinzi.wanakumbali kukaa siku nzima wakimsubiri kiongozi wao huku wakiumizwa na jua hilo.
- ✓ Sugu anakosa washirika katika hafla ya kuapishwa,licha ya kuwalipia nauli ya ndege viongozi wa majimbo jirani.Huu ni msiba wa kujitakia ,kwani hatilii maanani maslahi ya wananchi.anataka kuwatumbuiza viongozi kutoka nje kwa fedha za walipa ushuru.hali hii pia inatokana na ushindi wake anaopata kupitia mlango wa nyuma.

(6x2=12)

**8.**
**a.**

i. Taswira-lililokuwa likielekea mwambani
ii. jazanda-kukitia kichwa chake kinywani mwa samba
iii. swali balagha.-lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?
iv. nahau- kuliokoa jahazi

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**b.**

i.ufisadi umekithiri katika nchi ya Matuo. Watu wenye ushawishi kama Sagilu hawakulipa kodi na waliagiza hata bidhaa hatari kama maziwa ya watoto yenye sumu.
ii.Kulikuwa na ukabila. Mangwasha anaeleza jinsi waajiiwa wengi katika ofisi ya chifu walikuwa wa kabila lake mshabaha.
iii. Ubaguzi katika ajira. Utawala wa mtemi unawabagua waketwa wakati wa ajira.
iv.Uhaba wa ajira. Vijana wengi waliokuwa wamehafilika kutoka taasisi za elimu walikosa kazi.
v. Ukiritimba wa kiuchumi. Sagilu anamiliki nyenzo zote muhimu za kiuchumi
vi. Unyakuzi wa mali ya umma. Nanzia ananyakua jengo moja refu katikati ya mji.
vii. Unyakuzi wa ardhi ya wanajamii. Sagilu napanga kunyakua ardhi ya wanamatango.
viii. Kufutwa kazi kiholela. Mangwasha anapigwa kalamu katika ofisi ya chifu kwa kuunga mkono kampeni za Lonare.
ix. Mshahara mdogo kwa wafanyikazi. Mshahara anaolipwa Mangwasha haukuhudumia familia yake.
x. Ukosefu wa elimu miongoni mwa vijana. Mangwasha aliwaona vijana wakizurura mtaani.
xi. Kutelekeza watoto wa kiume na kuishia kuingilia matumizi ya dawa za kulevya.
xii.Watoto wa kike wanatumiwa katika biashara ya ngono. Sihaba anamiliki danguro anapotumia wasichana wadogo.
xiii. Ulanguzi wa mihadarati. Ngoswe namiliki mtandao wa ulanguzi wa dawa za kulevya.
xiv. Matumizi ya pombe haramu. Mrima wanabugia pombe harmu
xv. Ukware. Sagilu anajihusisha kimapenzi na Cheiya ingawa ana mke.
xvi. Utekaji nyara. Utawala wa Lesulia unamteka nyara Lonare ili asishindane naye katika uchaguzi.
xvii. Uharibifu wa mazingira. Viongozi walichimba mchanga na kukata miti bila kujali.

**c**.

i. Lonare ni kelelezo cha viongozi waadilifu. Hashiriki katika maovu ya wanasaiasa
ii. Anaonyesha changamoto za wakombozi katika jamii k.v kutekwa nyara
iii. Kielelezo cha unyenyekevu licha ya kuwa katika tabaka la juu.
iv. Anachimuza maudhui ya mshikamano wa kijamii. Anashirikiana na Mangwasha kumtafuta Mrima
v. Ni kelelezo cha wanaharakati wasiokata tama licha ya changamoto.
vi. Kielelezo cha uwajibikaji katika malezi.
vii. Amejenga maudhui ya utu na ukombozi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes